



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
TUME YA TAIFA YA UCHAGUZI



TAARIFA KWA UMMA KUHUSU UCHAGUZI MDOGO WA
KATA 23 ZA TANZANIA BARA

Dodoma, 15 Februari, 2024

Tume ya Taifa ya Uchaguzi imepokea taarifa kutoka kwa Waziri mwenye dhamana ya Serikali za Mitaa, akiitaarifu kuhusu uwepo wa nafasi wazi za madiwani katika kata 23 za Tanzania Bara. Waziri ametoa taarifa hiyo kwa kuzingatia matakwa ya kifungu cha 13(1) cha Sheria ya Uchaguzi ya Serikali za Mitaa, Sura ya 292.

Kwa kuzingatia matakwa ya kifungu cha 13(3) cha Sheria ya Uchaguzi ya Serikali za Mitaa, Sura ya 292, Tume inatoa taarifa kwa umma kuhusu uwepo wa uchaguzi mdogo wa madiwani katika kata 23 za Tanzania Bara.

Ratiba ya uchaguzi mdogo utakaofanyika ni kama ifuatavyo:

- i. Fomu za uteuzi zitatolewa kuanzia tarehe 27/02/2024 hadi 04/03/2024;
- ii. Uteuzi wa wagombea katika uchaguzi huo utafanyika tarehe 04/03/2024;
- iii. Kampeni za uchaguzi zitafanyika kuanzia tarehe 05/03/2024 hadi 19/03/2024;
na
- iv. Uchaguzi utafanyika tarehe 20/03/2024.

Kata zinazohusika na uchaguzi huo mdogo ni kutoka halmashauri 21 zilizopo katika mikoja 15 kama ifuatavyo:-

Na.	Mkoa	Halmashauri ya	Kata
1.	Dar es Salaam	Manispaa ya Kigamboni	Kimbiji
2.	Kigoma	Manispaa ya Kigoma/Ujiji	Kasingirima
3.	Tabora	Manispaa ya Tabora	Ndevelwa
4.	Pwani	Mji Kibaha	Msangani
		Wilaya ya Bagamoyo	Fukayosi
		Wilaya ya Kibiti	Mlanzi
5.	Ruvuma	Mji Mbinga	Utiri
		Wilaya ya Songea	Mbingamhalule
6.	Geita	Wilaya ya Mbogwe	Isebya
7.	Lindi	Wilaya ya Kilwa	Kibata
8.	Mara	Wilaya ya Musoma	Mshikamano
		Wilaya ya Butiama	Busegwe
9.	Mbeya	Wilaya ya Kyela	Nkokwa
10.	Morogoro	Wilaya ya Mlimba	Kamwene
11.	Mtwara	Wilaya ya Nanyumbu	Chipuputa
12.	Mwanza	Wilaya ya Sengerema	Buzilasoga
		Wilaya ya Kwimba	Mhande
13.	Rukwa	Wilaya ya Nkasi	Kabwe
14.	Simiyu	Wilaya ya Meatu	Bukundi
15.	Tanga	Wilaya ya Muheza	Mkuzi
		Wilaya ya Mkinga	Boma
			Mtimbwani

Na.	Mkoa	Halmashauri ya	Kata
			Mayomboni

Tume inatumia nafasi hii kuvikumbusha vyama vya siasa, wagombea na wadau wote wa uchaguzi kuzingatia Katiba, Sheria, Kanuni, Maadili ya Uchaguzi, Taratibu, Miongozo na maelekezo ya Tume katika kipindi cha uchaguzi huu mdogo.



Kailima, R. K.

MKURUGENZI WA UCHAGUZI